

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Dar es Salaam
30 Machi, 2026

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

RAIS SAMIA APOKEA RIPOTI ZA CAG, TAKUKURU NA PPRA, ASISITIZA UWAJIBIKAJI NA ULINZI WA RASILIMALI ZA TAIFA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amepokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Taarifa ya Utendaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), na Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji Kazi wa Ununuzi wa Umma, katika hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Rais Dkt. Samia amesisitiza umuhimu wa uwajibikaji, uadilifu na usimamizi madhubuti wa rasilimali za umma, akieleza kuwa misingi hiyo ni nguzo muhimu katika kuimarisha utendaji wa Serikali na kuharakisha maendeleo ya Taifa.

Aidha, Rais Dkt. Samia amepongeza kazi inayofanywa na taasisi hizo katika kuimarisha uwazi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, akisema juhudi hizo zinaendelea kulinda rasilimali za Taifa na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

“Nimesikiliza taarifa zilizowasilishwa na taasisi zetu, na ninaendelea kuisitiza kuwa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma si jambo la hiari, bali ni wajibu wa msingi kwa kila kiongozi na mtumishi wa umma,” amesema Rais Dkt. Samia.

Akiizungumzia Ripoti ya CAG, Rais Dkt. Samia amesema tathmini hiyo ni nyenzo muhimu ya kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma, akibainisha kuwa Serikali imepokea na itazifanyia kazi hoja za ukaguzi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kwa upande wa ripoti za TAKUKURU na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Rais Dkt. Samia amesema zimeonesha hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, kuongeza uwazi katika manunuzi ya umma na



kuimarisha nidhamu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, akibainisha kuwa juhudi hizo ni muhimu katika kulinda rasilimali za Taifa na kuimarisha utawala bora.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amepongeza matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST), akisema umeongeza uwazi na ushindani katika manunuzi ya Serikali, sambamba na kuagiza kuimarishwa kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma. *“Tuendeleo kuimarisha mifumo ya kidijitali na ya usimamizi ili kuongeza uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma,”* amesema Rais Dkt. Samia.

Wakati huohuo, Rais Dkt. Samia amekemea vitendo vya uzembe, ubadhirifu na matumizi yasiyo sahihi ya rasilimali za umma, na kuonya dhidi ya vitendo vya makusudi vinavyokwamisha juhudi za maendeleo ya Taifa.

“Kila kiongozi na mtumishi wa umma ana wajibu wa kuhakikisha rasilimali za Taifa zinasimamiwa kwa uadilifu, kwa manufaa ya wananchi na maendeleo ya nchi yetu,” amesisitiza Rais Dkt. Samia.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia amezitaka taasisi za umma kuchukua hatua kwa wakati kushughulikia hoja zilizobainishwa, akisisitiza kuwa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti hizo utaimarisha uwajibikaji, kulinda rasilimali za Taifa na kuongeza ufanisi wa Serikali katika kuwahudumia wananchi.

TAARIFA KWA MHARIRI:

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imeonesha kuwa deni la Taifa linaendelea kuwa himilivu, likizingatia uwezo wa Serikali kulihudumia pamoja na mwenendo wa ukuaji wa uchumi na mapato ya ndani. Ripoti hiyo pia imebainisha ongezeko la hati safi kwa taasisi za umma, hali inayoashiria kuimarika kwa uwajibikaji, uwazi na usimamizi wa rasilimali za umma.

Kwa upande wa ununuzi wa umma, kwa mara ya kwanza Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji Kazi wa Ununuzi wa Umma imewasilishwa kwa Rais, hatua inayolenga kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.



Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu